THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
Kenya Certificate of Secondary Education

# 102/3 – KISWAHILI – Karatasi ya 3

PDF Compressor Free Version

## FASIHI

## Apr. 2021 – Muda: Saa 2½

Jina ............................................ Nambari ya Mtahiniwa ........................................

Sahihi ya Mtahiniwa ............................ Tarehe ..................................................

### Maagizo

(a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(c) *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*
(d) *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***lazima****.*
(e) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu* ***nne*** *zilizobaki; yaani: Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.*
(f) *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka* ***sehemu moja****.*
(g) *Majibu yote* ***lazima*** *yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
(h) *Majibu yote* ***sharti*** *yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
(i) ***Karatasi hii ina kurasa 24 zilizopigwa chapa.***
(j) ***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | Jumla | |

© 2020 The Kenya National Examinations Council



910187

Geuza ukurasa

Teacher.co.ke
Download Notes & More Free Revision Materials at https://teacher.co.ke/notes

## SEHEMU A: HADITHI FUPI

PDF Compressor Free Version

**A. Chokocho Na D. Kayanda:** *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*

Teacher.co.ke

**1. Lazima**

*D. Kayanda:* "Mwalimu Mstaafu"

(a) "Naomba radhi *mfawidhi* ... lakini nadhani ni jambo la busara kutokitia mchanga kitumbua..."

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Bainisha toni ya dondoo hili. (alama 2)

(iii) Kwa kurejelea hadithi hii jadili kwa kutoa hoja **kumi** namna mhusika Jairo alivyokitia kitumbua mchanga. (alama 10)

(b) Bainisha vipengele vya kimtindo katika dondoo lifuatalo: (alama 4)

"Alijaaliwa mvi nyeupe zilizojianika kwenye kichwa chake kidogo kilichosimama *jadidi* kwenye shingo yake nyembamba. Alijaaliwa mvi kwa vile zilikuja mapema wakati akiwa bado ana umri wa miaka thelathini. Watu wakasema hekima hiyo *kutabasuri* huko. Kwa hiyo, hakujisumbua kujipaka rangi nyeusi kuung'ang'ania ujana uliotishia kumwondoka mapema ... mvi zimemkaa kwa haiba kama theluji..."

## SEHEMU B: RIWAYA

**A. Matei:** *Chozi la Heri*

*Jibu swali la 2 au la 3*

**2.** (a) "Mara moyo unaanza kumwenda mbio na vipapasio vya akili yake kusimama wima. Anajihisi kama anayetarajia kuanza kinyang'anyiro kikali cha upiganaji masumbwi. Kwa mbali anasikia mbisho hafifu ... Anatoka nje kwenda kuitikia mbisho huu ... Mara anasikia moyo wake ukimwambia, "Yako ya arobaini imefika,"...

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Jadili aina **mbili** za taswira katika dondoo hili. (alama 2)

(iii) Bainisha vipengele vingine **vinne** vya kimtindo katika dondoo hili. (alama 4)

(b) Jadili umuhimu wa mandhari katika kuijenga riwaya hii kwa kurejelea kituo cha afya cha Mwanzo Mpya. (alama 10)

Download Notes & More Free Revision Materials at https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

PDF Compressor Free Version

**3.** (a) Changanua mtindo katika kifungu kifuatacho: (alama 8)

Wakati kama huu Mwangeka angejitanua kifua na kusema, "Mimi ni mwana wa mhunzi, na bila shaka wa mhunzi asiposana huvuvia. Babangu hakuna linalomshinda katika uwanja wa upasuaji. Ni kama yule mbabe wa kivita aliyepigana na *Akavi* kuwaokoa mifugo wa ukoo wetu kutokana na kutekwa na jamaa hawa ambao siku hizo wakiamini ndio waliotunukiwa na Manani jukumu la kuwamiliki ng'ombe wote. Baba huniambia kuwa mara nyingi huwafufua maiti katika chumba cha wagonjwa mahututi, akawatoa kwenye mashine na kuwarejeshea uhai, jamaa zao wakitazama hivi hivi! Hilo usilione dogo, Tet! Baba si tofauti na huyo Fumo Liyongo tuliokuwa tukihadithiwa na nyanya. Ati bwana huyu angeweza kuinua tani ngapi vile za chuma?"

"Mia moja!" Mwangemi angemkumbusha mwenzake kila mara.

(b) Kwa kurejelea kisa kinachosimuliwa kuhusu Mwangeka, Mwangemi na babu yao, jadili mchango wa familia katika kuendeleza desturi za kijamii. (alama 12)

## SEHEMU C: TAMTHILIA

**P. Kea:** *Kigogo*

*Jibu swali la 4 au la 5*

**4.** "Nilijua ninawaponza, nilijua ninawapunja, nilijua ninawadhuru ... lakini nilimezwa na tamaa."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Bainisha vipengele **viwili** vya kimtindo katika dondoo hili. (alama 4)

(c) Fafanua umuhimu wa mzungumzaji katika kuvijenga vipengele vifuatavyo vya tamthilia hii.

(i) Ploti (alama 6)

(ii) Maudhui (alama 6)

**5.** (a) Jadili mchango wa wasomi katika hali ya maisha ya Wanasagamoyo. (alama 10)

(b) Fafanua umuhimu wa mazungumzo kati ya Majoka na Daktari katika kujenga tamthilia ya *Kigogo*. (alama 10)

Download Notes & More Free Revision Materials at https://teacher.co.ke/notes

## SEHEMU D: USHAIRI

PDF Compressor Free Version

*Jibu swali la 6 au la 7*

Teacher.co.ke

**6.** *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Mruka juu kipungu, hurejea ardhini
Yasemwa tangu tangu, zamani hizo zamani
Ukweli jua mchungu, hili mja ubaini
Mpanda ngazi jamani, hakwei ili kushuka.

Muhali hili nasema, mpanda ngazi kushuka
Utabaki kutazama, kama ataporomoka
Hapo juu kagandama, kileleni amefika
Mpanda ngazi jamani, kurudi chini hawezi.

Kurudi chini hawezi, hili jambo muhali
Ameotesha makwezi, apania kwenda mbali
Angani ndio makazi, *kuanisi* kila hali
Mpanda ngazi jamani, kushuka chini haramu.

Kushuka chini haramu, hili bado nakariri
Twabaki kumhukumu, mkwezi huyu mahiri
Usingoje kwa hamumu, zapita nyingi *dahari*
Mpanda ngazi jamani, amebaki kileleni.

Amebaki kileleni, hukohuko anaketi
Daima yu furahani, hapati shida katiti
Walo chini mashakani, walia zao nyakati
Mpanda ngazi jamani, amepanda akapanda.

Amepanda akapanda, walio chini wa chini
Umpinge ukipenda, ila hili libaini
Mpanda ngazi kapanda, harudi tena badani
Mpanda gazi jamani, hatashuka kwa hiari.

Hatashuka kwa hiari, jinsi anavyoanisi
Wala haoni hatari, katu hana wasiwasi
Anaishi kwa fahari, ni nyofu yake nafasi
Mpanda gazi jamani, hakwei ili kushuka

Hakwei ili kushuka, kuacha yake makao
Ameshika kwa hakika, mashiko penye *mafao*
Amepanga kaka kaka, kuchuma mengi mazao
Mpanda ngazi jamani, kuija chini hashuki.

Download Notes & More Free Revision Materials at https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

Kuija chini hashuki, mti ungaporomoka
Tumpige kwa mikuki, ngawiraye kumpoka
Atahapa haki haki, si halali kwa hakika
Mpanda ngazi jamani, harudi katu harudi.

PDF Compressor Free Version

Harudi katu harudi, kurudi chini tulipo
Apigwe pigo ja radi, atabaki papo hapo
Bado azidi kaidi, kuapa kila kiapo
Mpanda ngazi jamani, hakwei ili kushuka.

(Kitula K.)

(a) Fafanua, kwa hoja **sita** mtazamo wa nafsineni kuhusu mpanda ngazi kwa mujibu wa shairi hili. (alama 6)

(b) Eleza aina **nne** za taswira zinazojitokeza katika shairi hili. (alama 4)

(c) Bainisha aina **tatu** za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 3)

(d) Huku ukitoa mifano, onyesha mbinu **mbili** ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 2)

(e) Bainisha mbinu zifuatazo za kimtindo katika shairi hili: (alama 3)

(i) Tanakuzi

(ii) Chuku

(iii) Sitiari

(f) Eleza muundo wa ubeti wa **tisa** na **kumi**. (alama 2)

Download Notes & More Free Revision Materials at https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

7. *Soma Shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

PDF Compressor Free Version

U wapi ujana wangu, na madhubuti ya nia?
Niko hapa peke yangu, ujana umepotea
Umeanacha na machungu, mambo niliyozoea
Kuwa na uwezo wangu, leo hayawezi kuwa
Afya ya ujana wangu, nayo imeshika njia,
Siku za ujana wangu, nazo sizioni pia,
Nadhari sasa si yangu, tazama hii dunia!

U wapi ujana wangu, ubingwa na mazoea?
Ndugu za jamaa zangu, na watu niliojua,
Wamehama ulimwengu, ni pweke nimebakia
Nguvu wanazo wenzangu, sasa wanazitumia
Nikishikacho si changu, ajabu hii dunia.
Hutia kizunguzungu, wakati wa kuchungua
Kama hukumbuki Mungu, kufuruni utakuwa.

U wapi ujana wangu, na maringo ya tabia?
Hamna kinywani mwangu, jino lililobakia,
Na laini gumu kwangu, sina cha kutafunia
Kitamu sasa kichungu, hata kama ni halua
Kama ningefungwa pingu, sina la kufurahia
Katika maisha yangu, nimebaki na fadhaa
Kama fumbo ulimwengu, na watu wazuzuliwa.

(S. Robert)

(a) Bainisha kwa hoja **tano** kinyume kinavyojitokeza katika shairi hili. (alama 5)

(b) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)

(c) Eleza aina **nne** za taswira katika shairi hili. (alama 4)

(d) Onyesha mifano ya mbinu zifuatazo katika shairi hili: (alama 4)

(i) Kweli kinzani

(ii) Tashihisi

(iii) Tasfida

(iv) Usambamba

(e) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 1)

(f) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)

Download Notes & More Free Revision Materials at https://teacher.co.ke/notes

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8.** *Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.*

PDF Compressor Free Version

Zamani sana Sungura na Fisi walikuwa marafiki wa kufa kuzikana. Mjukuu wangu sijui kama umewahi kuuwazia urafiki wa aina hii; ule wa mmoja wao akijikwaa dole anayeuhisi uchungu wenyewe ni mwenzake.

Siku moja walialikwa karamuni na Tumbili. Marafiki hawa waliafikiana waandamane asubuhi na mapema. Hata hivyo, Fisi alipofika nyumbani kwake moyo wake ulimrai, "Ndugu, wewe unajua mambo ya akutanguliaye chanoni hukuzidi tonge, na atanguliaye kisimani hunywa maji maenge? Itakuwaje umngojee Sungura na hali kimo chake ndicho hicho? Hata akafika amechelewa atakula shibe yake; wewe unahitaji kutwa nzima kulijaza tumbo lako kuza. Wewe jihimu mapema, huyu mwenzako atakufuata."

Asubuhi na mapema Fisi alishika tariki...guu mosi guu pili... guu mosi, guu pili ... hadi kwa Tumbili. Harufu nzuri ya mapochopocho ilihanikiza hewa; harufu ambayo ilimfanya Fisi kuchezesha midomo yake hivi na mate kudondoka ndo ndo ndo! Fisi alifika karamuni na kuchukua nafasi katika viti vya mbele asije akapitwa na chochote.

Nyuma kule Sungura alipitia kwa Fisi lakini hakumpata.

"Lo, kiumbe huyu!" Sungura alimwuliza Fisi kimoyomoyo, "utaacha lini tabia hii ya usaliti?" "Lazima nikukomeshe!"

Sungura alipofika karamuni alikaa kule nyuma akiwazia la kufanya. Fisi ambaye hakuwa na mwao na yaliyokuwa akilini mwa Sungura alimwendea na kumwambia, "Ndugu yangu, mtu huhifadhi akipatacho. Sijui kama nitawahi kuambulia shibe ya aina hii. Je, waonaje tukichukua baadhi ya vyakula hivi tupeleke nyumbani?"

Sungura alimwambia, "Hamna haja kujidhalilisha. Njia mufti ya kuhakikisha hutaona njaa tena ni kuhifadhi kilicho tumboni. Basi nitatumia ujuzi wangu wa utabibu kukusaidia kukitunza chakula tumboni. Fisi alikubali haraka.

Fisi alilia kwa maumivu makali lakini alipofikiria kuhusu kile chakula alivumilia huku mwili mzima unamtetema. Sungura alikamilisha mpango wake na kutwaa tabasamu la ushindi.

Basi mjukuu wangu, Sungura aliutwaa uzi na sindano ambayo alikuwa kaihifadhi kwenye kijaluba, akaanza kuupitisha ule uzi polepole – ee kwenye msamba wa Fisi. Fisi alilia kwa maumivu makali lakini alipofikiria kuhusu kile chakula alivumilia huku mwili mzima unamtetema. Sungura alikamilisha mpango wake na kutwaa tabasamu la ushindi.

Baada ya muda Fisi alirejea kubugia sahani za vyakula na mifupa bila kufanya nadhari. Polepole maumbile yalianza kudai haki, naye akatanabahi kwamba Sungura alikuwa kamnyima uwezo wa kuyatoshelezea maumbile haja. Alihangaza macho huku na kule, asimwone Sungura. Alijikokota mithili ya ng'ombe anayechungulia kaburi hadi kwa Sungura

Teacher.co.ke

PDF Compressor Free Version

Alimsihi Sungura amwondolee udhia huu lakini Sungura alikataa katakata, akamwambia "Jikune ujipatapo." Na kweli Fisi alijikuna ajipatapo. Kabla Sungura hajafumba jicho, alisikia kilio cha kite, kisha mpasuko mkubwa. Sungura aliangua cheko kubwa la stihizai na kumsukuma Fisi kutoka nyumbani kwake huku amefunika mianzi yake ya pua kwa viganja. Huo ukawa mwisho wa urafiki wa Sungura na Fisi. Tangu wakati huo, Fisi yumo mbioni kumtafuta Sungura ili amwadhibu.

Hadithi yangu imeishia hapo. Naomba ng'ombe wangu wafaidi nyasi za kijani na wako wafe kwa kiangazi.

(a) Onyesha kwa nini hii ni ngano ya usuli. (alama 2)

(b) Fafanua vipengele **kumi** vya kimtindo ambavyo fanani ametumia kufanikisha uwasilishaji wake. (alama 10)

(c) Eleza umuhimu wa fomyula ya mwisho katika ngano hii. (alama 3)

(d) Wewe ni kati ya wanaotambiwa ngano ya aina hii. Fafanua mambo **matano** ambayo wewe na wenzako mnaweza kuchangia wakati wa utambaji. (alama 5)

Download Notes & More Free Revision Materials at https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

PDF Compressor Free Version

PDF Compressor Free Version

Teacher.co.ke

Download Notes & More Free Revision Materials at https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

PDF Compressor Free Version

Download Notes & More Free Revision Materials at https://teacher.co.ke/notes

PDF Compressor Free Version

Teacher.co.ke

Download Notes & More Free Revision Materials at https://teacher.co.ke/notes

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.